


Hapo zamani za kale kijiji cha Mwese kilikuwa na rutuba tele. Watu hawakuwa na hofu ya wanyama waharibifu kama Nyani, Ngedere na Kware. Matunda ya porini yalikuwa mengi na majani kwa wanyama yalikuwa mengi. Wanakijiji wa Mwese walikuwa wakulima hodari. Walilima mahindi, karanga, mpunga, kunde, maharage, choroko, viazi na mihogo.

Mwaka mmoja mvua ilikuwa haba, mazao yao yalidhoofika kwa jua. Hawakuwa na mazao mengi kama miaka iliyopita. Wanyama nao wakaanza kutafuta chakula na maji. Nyani waliingia mashambani na kula mahindi.

Wanakijiji wa Mwese walijitahidi sana kuwafukuza kwa mishale na mawe, lakini Nyani hawakuondoka. Walikimbia tu, mara walipoona wanakijiji wameondoka, walirudi tena shambani.

Mzee Malele alikuwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Mwese. Aliwaambia wenzake, “Jamani, ninafikiri sasa tuanze zamu ya ulinzi, tulinde usiku na mchana ili kulinda mazao yetu.”

Wanakijiji walikubaliana na wazo la Mwenyekiti Mzee Malele. Zamu zilipangwa kwa kila mmoja, wanawake kwa wanaume. Walioachwa ni watoto, wazee na wagonjwa tu. Kila mwanakijiji alishika zamu yake barabara akiwa na silaha zote.


Nyani waliona sasa hakuna ujanja tena, kwani wanadamu wako kila wakati shambani na hivyo walishindwa kuiba mahindi kwa muda mrefu. Nyani walipoona sasa watakufa kwa njaa, walikusanyika ili waamue nini cha kufanya.

Baada ya kufikiri na kujadili sana, walipata wazo waliloona linafaa. Waliamua wamkate mkia mmoja wao, kisha wamvalishe nguo ili aonekane kama binadamu na akaombe kazi ya ulinzi katika Kijiji cha Mwese.

Sharti lake ni moja lazima awaachie nyani wote kula mahindi kila watakapokuja shambani. Asubuhi nyani wote walikusanyika ili achaguliwe ambaye atakatwa mkia. Mmoja wao ambaye alionekana jasiri alichaguliwa na kukatwa mkia.

Baada ya wiki mbili yule nyani alikuwa amepona na alipewa jina la Bwana Maseleni. Walimvalisha nguo Bwana Maseleni, naye akawa kama binadamu. Walizidi kumwusia kuwa asisahau ahadi waliyowekeana. Naye akaahidi kutunza ahadi hiyo na kuwa sasa wajue kuwa njaa hakuna tena, kwani atawaruhusu kula mahindi kama wanavyotaka.

Baada ya matayarisho alianza safari ya kwenda kijijini Mwese kuomba kazi ya ulinzi. Baada ya mwendo mfupi, Bwana Maseleni alikutana na kundi kubwa la wanakijiji waliokuwa wanakwenda kulinda mazao yao.



Bwana Maseleni, aliwasalimia na alijitambulisha kuwa yeye ametokea katika Kijiji cha Mapori amekuja hapo kuomba kazi ya ulinzi. Wale wanakijiji wakamwambia aende hadi kijijini atakutana na chifu, akamweleze shida yake.

Kule kijijini Bwana Maseleni akakutana na chifu wa kijiji na kumweleza nia yake, Chifu Jumbe akawaita wajumbe wa baraza na kumjadili. Baada ya majadiliano, walikubaliana kuwa apewe kazi ya ulinzi na atakuwa anakaa kwa Chifu Jumbe kwa uangalizi zaidi.

Bwana Maseleni alianza kazi yake ya ulinzi mara mmoja. Bila hata ya kugundulika alifanya kazi yake vizuri sana. Nyani kila walipokuja shambani aliwafukuza, hata hakujali ile ahadi waliyowekeana. Waliporukia kwenye miti, na yeye alipanda kwa ustadi mkubwa sana, alipowakamata aliwapiga bila huruma kama hawajui.

Wanakijiji walimpenda sana mlinzi wao. Waliamua kumuongezea ule mshahara wake mara mbili ya aliokuwa anapata hapo awali. Nyani waliacha kabisa kufika mashambani, walihofia kukamatwa na kupigwa na Nyani mwenzao waliyemtuma. Kule msituni nyani wote walidhoofika sana kwa sababu ya njaa.

Hali ilipokuwa mbaya waliitisha mkutano. Waliamua kumtuma Nyani mmoja aende katika Kijiji cha Mwese kwa siri. Lengo la safari yao ni kumkumbusha Bwana Maseleni ahadi waliyowekeana.

Pia, walimtuma akamwabie kuwa asipojirekebisha, watamrudishia mkia wake. Habari zilipomfikia Bwana Maseleni, akajifanya hasikii. Akamwambia yule nyani, “Nenda ukawaambie kuwa wasinijue na mimi sio nyani, mimi sasa ni mkuu wa walinzi wote.”

Yule mjumbe alipeleka taarifa hizo kwa nyani wenzake. Baada ya kusubiri muda mrefu bila mafanikio ya kupata chakula, waliamua waende kijijini wakamrudishie mkia wake.


Walifanya mkutano wa jinsi ya kwenda kijijini na kumrudishia mkia wake. Waliamua kwenda siku inayofuata asubuhi. Siku iliyofuata asubuhi na mapema nyani wote walitoka na kwenda katika Kijiji cha Mwese.

Baada ya muda wanakijiji waliamshwa na kelele za nyani walipotoka nje wakaona vumbi linatimka na nyani wengine wanakuja wakicheza na kuimba.
Bwana Maseleni
Kiitikio: Tumpe mkia wake tukampe x 2
Ti ti tiii
Kiitikio: Tukampe mkia wake tukampe x 2

Wanakijiji waliposikia walishangaa, kuusikia wimbo huo. Bwana Maseleni alipousikia wimbo nae akajua kuwa sasa siku za mwizi ni arobaini. Alianza kuhangaika sana. Watu wote wa kijijini walianza kukimbia kuelekea kwa Chifu Jumbe. Ambako kundi la nyani lilikokuwa linaelekea. Kila mmoja alitoka na silaha yake.
Wanakijiji walianza kuwatupia mishale na mikuki nyani. Lakini Chifu Jumbe aliwakataza alisema, "Waacheni, huenda wana ujumbe lakini wakileta matata tutawashambulia." Walipofika katika uwanja wa nyumba ya Chifu Jumbe nyani wote wakanyamaza.

Mkuu wa nyani aliyeitwa Gendayeka alijitokeza mbele ya wote na kuanza kusema. "Sisi tumekuja kumrudishia mkia Bwana Maseleni. Maana yeye ni Nyani mwenzetu." Aliendelea kusema, "Tulimkata mkia na kumgeuza binadamu ili aturuhusu kula mahindi shambani. Lakini Bwana Maseleni amevunja mkataba. Kila akituona shambani anatufukuza kama hatujui na pia, hutupiga sana." Alimaliza kusema Gendayeka.

Chifu Jumbe na watu wote walishangaa sana. Chifu Jumbe aliamua Bwana Maseleni aitwe. Alipofika aliulizwa ukweli wa mambo yale yote yaliyoelezwa, naye hakuwa na la kusema alitazama chini tu.




Ghafla! Yule Nyani aliyeshika mkia alimrukia bwana Maseleni na kumchomeka mkia wake. Bila kupoteza wakati, nyani wote walimchukua Bwana Maseleni na kuondoka naye mbio mbio.

Bwana Maseleni alisikika akilia kuwa wamsamehe wasimrudishie mkia. Hakuna hata mmoja wao aliyemsikiliza, walitembea naye kwa haraka kuelekea msituni. Wanakijiji walistaajabu sana kwa yale yote yaliyotokea.


Kilichowafurahisha ni kuwa, mahindi yao yalikuwa yameshakauka na hivyo hakukuwa na hofu ya Nyani tena. Wanakijiji wa Mwese wakaendelea na ulinzi wao, na hawakutaka tena kuajiri mlinzi kutoka nje ya kijiji chao.

Chifu Jumbe alitangaza kuwa kila mmoja ataanza kulinda mazao hadi yakauke kabisa. Akatoa amri ya kumchunguza kwa makini kila mgeni anayefika katika kijiji hiki kuishi au kuomba kazi.



Chifu Jumbe alisema kuwa, hatua hii itawasaidia kuwabaini wageni wa kweli na sio wa kweli. Chifu pia aliwakumbusha wananchi kuwa mazao yatakapokauka, yatavunwa kwa umoja kama ilivyokuwa kawaida ya kijiji cha Mwese.

Tangu siku hiyo kila mwanakijiji wa Mwese alishika zamu yake ya ulinzi kama mwanzo. Watoto wa Kijiji cha Mwese walianzisha mchezo kila siku jioni. Walikuwa wanazunguka huku wakiimba na kucheza. Bwana Maseleni.
Kiitikio: Tumpe mkia wake tukampe x 2
Ti ti tiii
Kiitikio: Tukampe mkia wake tukampe x 2
Wanampa mmoja kamba mfano wa mkia na kuzunguka.



Wale nyani waliondoka na yule Bwana Maseleni. Walipofika porini wakampa adhabu ya kuwalinda wenzake. Hadi leo utaona kila lilipo kundi la nyani, yupo mmoja anabaki kwenye mti ili kuangalia usalama wa wenzake.

Ikitokea hatari yoyote, yeye huwapa taarifa wenzake. Mara moja utawaona nyani wote wanakimbia na kupanda miti kwa haraka.